**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI ANUAI NA. 269 YA 2022**

**TRANSPAPER (T) LTD ................................ MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**AIDA GODFREY MBOYA ............................... MJIBU MAOMBI**

## UMUZI MDOGO

**25.10 & 26.10.2022**

**Rwizile, J**

Mleta maombi anaomba Mahakama itengue uamuzi wake katika maombi Na. 183 ya 2021. Kwa muhtasari maelezo ni kwamba mleta maombi alifungua maombi ya marejeo yaliyosajiliwa kwa namba 183/2021. Maombi hayo yalipangwa kusikilizwa tarehe 05.07.2022 saa nne kamili asubuhi. Siku hiyo, kama ilivyo ada maombi yaliitwa kwa muda ulipangwa. Wakili wa mleta maombi hakuwepo Mahakamani. Kwa kuwa Wakili wa mleta maombi au mleta maombi mwenyewe hawakuwepo bila taarifa, maombi hayo yalifutwa.

Inasemekana wakili wa mleta maombi alifika baadae na kufahamishwa kuwa shauri lilifutwa. Maombi haya kwa hiyo, yalifunguliwa kuomba Mahakama kutengua amri ya kulifuta shauri hilo.

Maombi yameambatana na kiapo cha Wakili wa mleta maombi, kwa jina la Victoria G. Mgonja. Sababu ya maombi haya ni kama ifuatavyo: -

> *Kama mleta maombi ana sababu za msingi za kuifanya Mahakama iweze kurejesha maombi ya marejeo namba 183 ya mwaka 2021.*

Mleta maombi aliwakilishwa na Bi. Victoria G. Mgonja wakili msomi wakati mjibu maombi aliwakilishwa na wakili msomi Bwana Saulo Kusakalah ambaye aliyapinga maombi haya.

Katika wasilisho lake, wakili Mgonja aliiomba Mahakama kurejesha maombi ya marejeo Na. 183 ya mwaka 2021 ambayo yalifutwa tarehe 05.07.2022. Alisema sababu ni kwamba siku hiyo alikuwa anaumwa, akapitia zahanati, baada ya vipimo alikutwa anaumwa Malaria. Hivyo akachomwa sindano ya kushusha homa. Kuthibitisha hayo aliwasilisha cheti cha hospitali kama kielelezo ZB1. Aliendelea kueleza kuwa alipotoka hapo alifika mahakamani saa 4:30 asubuhi na akapewa taarifa kuwa shauri lilifutwa kwa kutokufika kwake. Hivyo akaomba shauri hilo kurejeshwa Mahakamani.

Katika kujibu, Wakili msomi Kusakalah alisema kuwa tarehe 05.07.2022 alionana na wakili wa mleta maombi Victoria Mgonja, asubuhi hapa Mahakamani kabla ya shauri kuitwa. Shauri lilipoitwa, wakili Mgonja

hakuwepo. Aliendelea kusema kuwa muda wa saa tano walipotoka walimkuta katika korido za Mahakama akijiandaa kuingia Mahakamani.

Alieleza pia kuwa shauri lililoondolewa liliitwa saa tano na hivyo sio kweli kwamba wakili huyo alifika saa 4:30. Kisha akaeleza kuwa hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa kweli asubuhi alikuwa hospitali kwakuwa kiambatisho ZB1 hakionyeshi hivyo. Kwa maelezo yake inawezekana wakili wa mleta maombi alikwenda zahanati jioni. Kwa mtazamo wake wakili angeleta angalau risiti ya EFD ambayo ingeonyesha muda aliokuwa zahanati.

Bwana Kusakalah aliwasilisha zaidi kuwa cheti kilichowasilishwa ni cha kupikwa na hakifai. Kwa mawazo yake cheti hicho kinaonyesha alikutwa na ugonjwa Malaria kwa kupimo cha mkojo. Alisema, hakuna popote panapoonyesha kwenye mkojo kulikuwa na usaha na hakuna kitu kinachofanana na hicho. Aliendelea kusema kuwa maelezo ya cheti hicho yanatia shaka, kwa sababu mtu mwenye kutapika, joto kali la nyuzi joto 38.9 asingeweza kufika mahakamani. Aliendelea kueleza kuwa kutokufika Mahakamani kunaweza kukubalika endapo kuna sababu za msingi, hivyo akaomba maombi yafukuzwe.

Katika mawasilisho ya nyongeza Bi. Mgonja alisema kuwa siku ya tarehe 05.07.2022 hakuonana na wakili wa mjibu maombi na wala hakuwa na shauri zaidi hilo. Mwisho aliiomba Mahakama kuyakubali maombi haya.

Baada ya kupitia mawasilisho ya pande zote mbili, Mahakama imeona hoja moja ya kujadili ya *endapo mleta maombi ameweza kuithibitishia Mahakama alikuwa na sababu za msingi kutofika Mahakamani kwa wakati uliopangwa*.

Kanuni ya 36(1) na ya 38(1)(a)(c) and (2) za Kanuni za Mahakama ya Kazi, TLS 106 ya 2007 zinaelekeza kwamba shauri linaweza kurudishwa Mahakamani baada ya mleta maombi kuonyesha sababu za msingi zilizopelekea kutokufika mahakamani katika tarehe ya kusikilizwa.

Mahakama katika kupitia kielelezo kilichofikishwa Mahakamani na wakili wa mleta maombi, yaani ZB1, imebaini kuonyesha siku ya tarehe 05.07.2022 wakili wa mleta maombi alikuwa zahanati akipatiwa matibabu lakini wakili wa mjibu maombi alibishania kielelezo hicho kwa kueleza kuwa kukosekana kwa risiti ya EFD kunafanya ushahidi huo kukosa mashiko kwakuwa risiti hiyo ingeonyesha muda halisi ambao wakili huyo alikuwa zahanati.

Mahakama inatamka wazi kuwa wakili wa mleta maombi ndie mwenye wajibu wa kuishawishi Mahakama kwa kuonyesha vielelezo vya kuridhisha ilimahakama iridhie kurudishwa kwa shauri lake.

Cheti cha zahanati (ZB1) kinaonyesha siku ya tarehe 05.07.2022 wakili wa mleta maombi alikuwa zahananti akitibiwa, na kama wakili wa mjibu maombi alivyowasilisha yawezekana tiba hiyo ilifanyika muda wowote isipokuwa mda ule wa shauri. Lakini pia wakili alisema alifika Mahakamani saa 4.30 na alikuta shauri limefutwa. Hakuna ushahidi huo na hivyo bado si salama kuamini alichokisema. Mahakama inaamini kuwa suala la ugonjwa ni sababu tosha ya kuahirisha shauri. Ilikufikia uamuzi huo, lazima mleta maombi athibishe kwanza bila shaka kwamba aliumwa kweli. Wakili wa mjibu maombi alisema cheti cha hospital kimegushiwa. Hata hivyo Mahakama ilielekeza cheti hicho kichunguzwe na taarifa kuletwa Mahakamani na Polisi wa Kanda Maalum. Inasikitisha mpaka tarehe ya umumuzi huu, taarifa ya uchunguzi haijaletwa.

Ni mtizamo wa Mahakama kwamba mleta maombi anapaswa kuthibitisha kutokuwepo kwake kwa wakati kulitokana na kuumwa. Kuleta cheti tu cha kuugua hakuthibitishi alikuwa hospitalini kwa muda ambao shauri liliitwa. Nidhahili, wakili Mgonja ameshindwa kuthibitisha hilo. Hivyo maombi haya hayana mashiko kwa kukosa sababu za msingi. Na hivyo yametupiliwa

mbali. Na kwakuwa hili ni shauri la mgogoro wa kikazi, kila upande utajilipia gharama zake.

**A.K. RWIZILE**

**JUDGE**

**26.10.2022**